



TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Benki Kuu ya Tanzania ilikutana tarehe 19 Novemba 2020 kutathmini mwenendo wa uchumi na mwelekeo wake katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Kamati imeridhishwa na mwenendo wa uchumi licha ya athari katika uchumi wa dunia zinazotokana na kuongezeka kwa maambukizi ya ugonjwa wa Corona katika baadhi ya nchi washirika wa biashara.

Kamati ya Sera ya Fedha imeridhika na kuendelea kuimarika kwa viashiria vya uchumi kulingana na viwango vilivyokubalika kitaifa na kikanda. Pato la Taifa liliendelea kuonyesha viwango chanya vya ukuaji, huku makadirio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2020 yakiwa ni asilimia 5.5. Kasi ya mfumuko wa bei ilibaki katika kiwango cha chini, ikiwa ni asilimia 3.1 mwezi Oktoba 2020, na unatarajiwa kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3 hadi 5 kwa kipindi kilichobaki cha mwaka 2020/21, kutokana na kuwepo kwa chakula cha kutosha, kiwango tulivu cha kubadilisha fedha na bei ndogo za mafuta katika soko la dunia. Sekta ya nje imeendelea kuimarika kutokana na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara kufuatia mataifa mbalimbali kuendelea kulegeza hatua zilizochukuliwa kukabiliana na ugonjwa wa Corona. Hali hii imewezesha ongezeko la mauzo nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kutosheleza mahitaji ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, kufikia miezi 5.8. Mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali umeendelea kuwa wa kuridhisha kutokana na kuendelea kuimarika kwa makusanyo ya kodi na usimamizi thabiti wa matumizi.

Aidha, mikopo ya benki kwa sekta binafsi ilikuwa kwa asilimia 5.2 mwezi Septemba 2020 ikilinganishwa na asilimia 9.3 katika mwezi kama huo mwaka 2019. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuongezeka katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2020/21 kutokana na sera wezeshi ya fedha na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Vilevile, sekta ya benki imeendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha kuwezesha shughuli za uchumi kuendelea kuimarika.

Vilevile, Kamati ya Sera ya Fedha ilijadili mwenendo wa uchumi wa dunia na kubaini kushuka kwa ukuaji wa uchumi kutokana na athari za janga la ugonjwa wa Corona. Athari hizo zinatarajiwa kupungua kutokana utekelezaji wa sera za kibajeti na sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi.

Kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi nchini na wa dunia, Kamati ya Sera ya Fedha imeielekeza Benki Kuu kuendelea na utekelezaji wa sera ya fedha ili kuongeza ukwasi kwenye uchumi. Sera hii inalenga kuwezesha uongezeko la utoaji wa mikopo kwa riba nafuu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Kamati imehimiza wadau wote kuwezesha kufikia matarajio yaliyokusudiwa ya mwelekeo wa sera ya fedha.

**Gavana
Benki Kuu ya Tanzania**